# <u>CHANGAMOTO NYINGINE KATIKA MAISHA YETU NI KWA AJILI YA UTUKUFU WA MUNGU (NI ILI YESU ATUKUZWE MBELENI)</u>

## <u>Maandiko: Yoh 9: 1 – 12, 24 – 34</u>

1. **<u>UTANGULIZI</u>**

   Kama nilivyosema katika siku za nyuma kwamba changamoto tunazokutana nazo ndizo wakati mwingine zimebeba baraka zetu; leo nataka nianze ujumbe wangu kwa kutoa rai tu kwamba, tunapomwona leo mtu anapitia katika dhiki fulani au mateso fulani; kama hatuwezi kumwombea ni **bora** tukanyamaza kabisa maadamu sisi hatujui kwa nini Mungu ameruhusu apitie kwenye jaribu/changamoto hiyo na pia hatujui mwisho wa jaribu/ changamoto hiyo ni nini!! **Ni bora kabisa tukanyamaza kimya ili tusije tukaaibika baadae/ mbeleni maana nimegundua katika safari yangu hii ya wokovu kwamba changamoto nyingine katika maisha ya watoto wa Mungu ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu mbeleni.** ***Ayubu 23: (10) na Ayubu 19: 25 – 27.***

***Note:*** **Mungu anaweza kabisa kuruhusu mtoto wake apitie changamoto fulani katika maisha yake ili ajipatie utukufu baadaye; na siyo kweli kwamba wote wanaopitia changamoto fulani katika maisha yao wametenda dhambi mbele za Mungu.** ***Yoh 11: 1 – 4.*** Ugonjwa hadi kifo cha Lazaro ilikuwa ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu baadae. ***Yoh 11: 45 - 48***

2. Jambo kubwa la kufanya tunapokuwa tunapitia katika chanagmoto fulani katika maisha yetu ni kuelewa kwa kina kwamba changamoto hizo kazi yake kubwa ni kuandaa Baraka zetu kubwa zilizo mbele yetu. ***Zab 23 :5 – 6***

- Siri hii ya Daudi ilinifungua macho sana katika maisha yangu baada ya kuielewa; Daudi alikuwa na picha baada ya kuwa amajawa Roho Mtakatifu na akajua kabisa kwamba mambo magumu anayoyapitia kwa miaka 13 yote ndiyo yanayoandaa baraka zake na utukufu mkubwa wa Mungu wake katika maisha yake.
- **Na huenda kabisa na sisi mateso tunayopitia kwa sasa na dhiki na matukano na keleji na dhihaka kwa Kanisa letu au wateule binafsi ndivyo vinavyoandaa utukufu mkubwa wa Mungu wetu kwa Kanisa lake, nchi yetu na kwetu binafsi.** ***Esta 6: 1 – 14, Neh 4: 1 – 3***
- **Baada ya jaribu hili, tutatoka kama dhahabu!!** Tusikubali kuyumbishwa na adui kutokana na vitisho vyake, bali kama Yesu alivyojaribiwa na akasimama imara na baadae kukirimiwa jina lipitalo majina yote, nasi tusimame tu katikati ya changamoto tunazokutana nazo katika ulimwengu huu maadamu Yesu Kristo hakutuficha. ***Ebr 5: 7 – 8, Filp 2: 5 – 11; Yoh: 16: 33, 17: 15.***
- Ayubu alikuwa na hakika kubwa ya moyoni kwamba baada ya changamoto kubwa anayopitia atatoka kama dhahabu!! Huu ni ufahamu wa hali ya juu kama alivyofahamu Daudi kwamba changamoto zake ndizo **zinazo andaa** baraka zake pamoja na utukufu mkubwa wa Mungu wake.

**Note:** Upofu wa kijana huyu ***Yoh 9: 1 – 4)*** ukawa ndiyo mlango wa Yesu kumtokea na kumfanya awe mhubiri wa injili kwa wazazi wake pamoja na wakuu wa dini ya wazazi wake na kwa vyovyote vile wazazi wake hawakubaki kama kwanza hata kama Biblia imenyamaza na haisemi jambo lolote zaidi kuhusu wao. ***Yoh 9: 18 – 23.*** **Kuzaliwa kipofu kukasababisha Yesu ajidhihirishe kwake na kisha kumtumikia kwa kazi yake ya kuhubiri injili halisi.** Shetani ni kama simba angurumaye; simba awindaye haungurumi maana wanyama wote

watakimbia, anapounguruma anatisha ili alale usingizi na changamoto nazo ziko hivyo hivyo, lengo lake ni kututishia. ***1Petro 5: 8 - 9***

3. Yesu anaweza asikusaidie/ asikujibu kwa haraka kama nilivyosema mwanzoni mwa ujumbe huu ili kupima imani yako kwake; lakini pia ili kuwanyamazisha wapiga filimbi mbeleni!! ***Math 15: 21 – 28; Math 9: 23 – 26.*** Kwa desturi ya hawa mataifa; kama msiba umehudhuriwa na wapiga filimbi ambao kazi yao ni kukoleza waombolezaji, basi msiba huo umepata heshima sana; hawa wapiga filimbi walikuwa wanakodishwa **(Flute players).** Yesu aliwaambia waondoke maana kijana hajafa **"walimcheka sana!!** Yesu alimponya, habari zake zikaenea katika katika nchi yao yote. Kifo cha kijana huyu kikafanya Yesu ajulikane katika nchi ile yote. (Wapiga filimbi – wahamasishaji ili watu walie wala hawana uhusisano kabisa na wafiwa!!!

- Hata Yesu aliponyamaza bila kumjibu huyu mama Mkananayo; wanafunzi wa Yesu walifunua mioyo yao ilivyo kwa kutojali shida za wanyonge na mwishowe wanabaki wakishangaa baada ya Yesu kusifia imani kubwa aliyokuwa nayo huyu mwanamke na Yesu akamponya binti yake. **Tujiepushe kabisa/ tunyamaze tunapomwona ndugu akipitia changamoto fulani katika maisha yake.**
- Hatuna sababu ya kuvunjika moyo wala kukatishwa tama na wapiga filimbi tu walio katikati yetu hata baada na maombi yetu kutojibiwa kwa haraka; ni saa ya kuwa makini mno maana changamoto tunazopitia ndiyo ngazi, ndiyo daraja la ushindi mkubwa ulio mbele yetu; na pia changamoto tunazopitia sasa ni kwa ajili ya Mungu kutukuzwa baadae.

**Note:** Yusuph alipitia changamoto ya kuchukiwa na ndugu zake na wakaamua kumuua ***(Mwz 37: 8 – 20)***

- Alifanya kazi ya **House boy!!** ***Mwanz 39: 1 – 6,***
- Alifungwa jela baada ya kukataa kutenda dhambi miaka 2. ***Mwanz 39: 13 – 23, 41: 1.*** "Yusufu alitumikia changamoto zote hizi kwa muda wa miaka **13 (Mwz 37: 2, 41: 46)** na anakuja kuonana na jamaa yake baada ya maiaka **22!!** Akiwa na umri wa **miaka 39!!** ***Mwaz 45: 1 – 15.*** Ona ufahamu aliokuwa nao Yusufu saa anapitia changamoto hizi – ***Mwaz 45: 4 – 8***
- Changamoto alizopitia Yusufu zikasababisha Mungu ajitukuze kwa Farao na hadi Farao kutambua kwamba Mungu wa Yusufu ni Mungu aliye hai. ***Mwaz 41: 37 – 40;*** na Yusufu kutukuzwa sana baadae na Bwana.
- Na sisi changamoto tunazopitia sasa ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu kesho. Amina

***Na***
***Askofu Dr. L. Mwizarubi***
***21/03/2021***